

# AUSCO

## Programu ya Maelekezo ya Kitamaduni nchini Australia

## KITABU CHA SHUGHULI




Australian Government
Department of Social Services

Inaletwa kwako na Shirika la Uhamiaji la Kimataifa kwa niaba ya Idara ya Huduma za Jamii nchini Australia

IOM • OIM

# Orodha ya yaliyomo

Kuanza . . . . . 2

Kitengo 1 Australia – maelezo ya jumla . . . . . 3

Kitengo 2 Kutulia nchini . . . . . 5

Kitengo 3 Makazi to Nyumba . . . . . 7

Kitengo 4 Afya . . . . . 9

Kitengo 5 Pesa . . . . . 11

Kitengo 6 Elimu . . . . . 13

Kitengo 7 Ajira . . . . . 15

Kitengo 8 Sheria . . . . . 17

Hadithi za Kutulia . . . . . 18

Rekodi ya Ustadi . . . . . 19

# Kuanza

Karibu katika utaratibu wa Programu ya Maelekezo ya Utamaduni nchini Australia (Australian Cultural Orientation Program - AUSCO). Lengo la AUSCO ni kukupa maelezo kuhusu safari yako nchini Australia pamoja na kujibu maswali yako mengi iwezekavyo kuhusu Australia.

Tuanze kwa kujua nini haswa WEWE unachotaka kujua. Tumia nafasi ya mstari iliyopo hapo chini ili kuandika maswali yako. Wakati unaposikia majibu ya moja wapo ya maswali yako wakati upo kwenye AUSCO, andika majibu hayo. AUSCO hukupatia wewe maelezo mengi na inaweza kuwa vigumu kukumbuka maelezo yote!

Mwisho wa programu, regelea tena maswali yako na uhakikishe kuwa unayo majibu yote unayohitaji. Wakati mwingine maswali yako yanaweza kuwa ngumu kujibiwa hadi unapowasili nchini Australia. Chukua pakiti lako la AUSCO unaposafiri Australia ili uweze kuendelea na kukusanya majibu ya maswali yako ambayo ni muhimu kwako.

## Maswali yako yanayohusu Australia ni yapi pamoja na makazi yako huko?

| Maswali | Majibu |
|---|---|
| | |
| | |
| | |
| | |
| | |
| | |
| | |
| | |
| | |
| | |
| | |
| | |
| | |
| | |
| | |
| | |
| | |
| | |
| | |
| | |
| | |
| | |
| | |
| | |

# **Kitengo 1** Australia – maelezo ya jumla

Australia ni nchi iliyo na fursa tele pamoja na uzoefu mpya.

Pia ni nchi kubwa sana, nchi kubwa ya sita duniani. Hii inamaanisha kuwa kila eneo la Australia ni tofauti. Katika upande wa kaskazini mwa Australia hali ya hewa ni tropikali, na kusini ni baridi kidogo.

Ingawaje Australia ni nchi kubwa, haina idadi kubwa ya watu – takriban watu milioni 23. Wengi wao huishi katika miji iliyokaribia ufuko wa bahari, lakini kunayo pia miji yenye ukulima iliyo barani. Jiji kuu la Australia, Canberra, lipo pia barani.

Wakati unapotulia katika maisha yako mapya nchini Australia utajifunza zaidi kuhusu maeneo tofauti nchini Australia. Kwa sasa, wewe utakuwa makini zaidi na jiji au eneo utakalotulia kwanza. Katika bunda lako la maelezo kutakuwemo ndani na vijifurushi vya maeneo tofauti nchini Australia.

## Shughuli

**Kulinganisha Australia na nchi zingine**

Tumia ramani ilipo hapo chini kuonyesha wapi utakapotulia wakati unapowasili nchini Australia.
Nchi yako ya nyumbani ni kubwa vipi ukilinganisha na Australia? Unaweza kuichora katika ramani hii?



Kwa njia gani ambazo eneo unalohamia ni sawa au tofauti na unapoishi sasa, au ulipoishi hapo awali?

Hali ya hewa?

Idadi ya watu?

Viwanda?

Taswira ya nchi?



Waaustralia hutokea sehemu zote za dunia. Asilimia arobaini na sita ya Waaustralia walizaliwa nchi za ng'ambo au wanaye mzazi aliyezaliwa nchi ya ng'ambo. Wameleta utamaduni tofauti, ambao wapo huru kuendeleza bali tu wasivunje sheria ya Australia.

Ni tabia, au mila na utamaduni gani umeshawahi kuona ambayo ni tofauti na mila au utamaduni wako wewe?

Unahisi vipi kuhusu tofauti hizi?

# **Kitengo 2** Kutulia nchini

Njia ya haraka ya kuishi katika Australia ni kupata kazi na kujifunza Kiingereza lakini kwa sababu wewe unawasili katika nchi mpya hii inaweza kuchukua muda. Baada ya kuwasili serikali inaweza kutoa baadhi ya misaada muhimu kukusaidia kuzoea maisha yako mpya.

Mfanyikazi wa kesi au mshauri wako atakusaidia wewe kupata huduma hizi.

## Shughuli

Kabla ya kuanza mada hii andika chini usaidizi gani wewe unaona utakaopewa unapowasili nchini Australia. Kwa kila maoni yako andika ni wapi ulipopata maelezo haya.

Kufikia mwisho wa mada hii tutaregelea maandishi yako ili kuona kama unahitaji kufanya mabadiliko yoyote.

| **Nafikiri nitapokea usaidizi huu ninapowasili nchini Australia** | **Ulipata wapi maelezo hayo?** | **Ulikuwa sahihi?** |
|---|---|---|
| Katika uwanja wa ndege | | |
| Nyumba | | |
| Pesa | | |
| Elimu | | |
| Afya | | |
| Vifaa vya nyumba | | |
| Manufaa/Marupurupu | | |
| Chakula | | |
| Kazi/Ajira | | |
| Utunzaji wa watoto | | |

## Shughuli

Je, unaweza kulinganisha huduma na mtoaji wake?

| | |
|---|---|
| **Caseworker** | Malipo kwa utunzaji wa watoto na usaidizi wa kimaisha |
| **Centrelink** | Madarasa ya kujifunza Kiingereza |
| **Medicare** | Vitabu, magazeti na gazeti la wiki katika lugha tofauti ili kuiazima |
| **Adult Migrant English Program (AMEP)** | Mtu atakayekusaidia ili utulie na upate huduma |
| **Translating and Interpreting Service (TIS National)** | Hutoa usaidizi kwa kulipia gharama za matibabu |
| **Special Broadcasting Service (SBS)** | Maelezo ya ukalimani ili wewe uweze kuyasikia katika lugha yako |
| **Public library** | Habari za redio na TV katika lugha nyingi |

# **Kitengo 3** Nyumba

Kunazo aina nyingi za makazi nchini Australia. Nyumba katika jiji huwa tofauti kuliko mitaa, na tofauti kuliko mji wa maeneo ya mbali. Labda nyumba hizi huwa tofauti na yale unazijua kutokana na uzoefu wako mwenyewe.

Gharama ya kupanga na kununua nyumba nchini Australia huwa juu sana. Wakati unapowasili kwa mara ya kwanza utahitaji kupanga nyumba.

## Shughuli

Hebu tulinganishe sehemu unapoishi sasa na sehemu unapoweza kuishi nchini Australia. Nafasi ya tatu ni yako kujaza wakati unapowasili nchini Australia!

| SASA | SASA | KATIKA MIEZI MIWILI |
|---|---|---|
| Unalipa pesa ngapi ili kuishi kwenye makazi unapoishi sasa? | Unafikiri utalipa pesa ngapi ili kuishi kwenye makazi nchini Australia? | UNALIPA pesa ngapi? |
| Makazi unapoishi sasa ina vyumba vingapi? | Unafikiri makazi utakapoishi nchini Australia itakuwa na vyumba vingapi? | UNAZO vyumba vingapi? |
| Makazi unapoishi sasa ina vifaa gani? | Unafikiri makazi utakapoishi nchini Australia itakuwa na vifaa gani? | UNAZO vifaa gani? |
| Unatarajia makazi yako kuwa bora, sawa au mbaya zaidi kuliko unapoishi sasa? Kwa njia gani? | | Je, makazi yako nchini Australia yanatekeleza matarajio yako? |

## Shughuli

Kunayo maneno mengine ya kisheria  iliyo muhimu unayofaa kujifunza ili kukusaidia wewe kujihisi upo na usukani wa jinsi ya kupangisha. Tafsiri maneno hayo kwenye lugha yako ili upate kuwa na orodha muhimu unayoweza kuregelea wakati unapowasili nchini Australia. Kiijifurushi cha maelezo kuhusu Nyumba yatakupa vidokezo.

| | |
|---|---|
| Lease | |
| Landlord | |
| Tenant | |
| Real estate agent | |
| Bond | |
| Utilities | |
| Condition report | |
| Inspection | |
| Accommodation | |

# **Kitengo 4** Afya

Australia inayo mfumo mzuri wa utunzaji wa afya lakini inaweza kufanya kazi kwa njia ambayo ni tofauti kutokana na jinsi ulivyozoea.

Wewe utapata utunzaji wa afya bure au ya ruzuku kupitia mfumo unaoitwa Medicare. Hata hivyo, huduma zingine kama vile daktari wa meno pamoja na kupata miwani ya macho huwa si bure.

Wewe utaweza Kumtembela daktari anayetibu magonjwa yote (General Practitioner - GP) au daktari kwa matibabu mengine yako zaidi. Ikiwa shida zako zinahitaji uangalifu zaidi ya mtaalamu watakupendekeza kwake Mtaalamu.

Hapa kunao mchoro ambao unaonyesha hatua tofauti ambazo zinaweza kutokea wakati unapomtembelea daktari.

Fuata hatua hizi na utambue wakati zinazokuwa tofauti kuliko mazoea yako ya Kumtembelea daktari.

Wakati unapojihisi mgonjwa, au wewe una shida ya matibabu hatua yako ya kwanza ni Kumtembelea daktari anayetibu magonjwa yote.

## Pigia simu daktari anayetibu magonjwa yote ili kupanga miadi

↓

Daktari anayetibu magonjwa yote ya kawaida anaweza kukusaidia kusuluhisha shida yako au kujibu maswali yako. Wanaweza kukupa maagizo ya kuchukua dawa zingine.

↓

Chukua maagizo yako ya dawa kwenye duka la dawa. Unaweza kungojea dakika 15 au kadhaa ili mfamasia atayarishe dawa zako.

Maelekezo ya kunywa dawa zako yatakuwa yameandikwa kwenye chupa au sanduku.

↓

Ikiwa daktari anayetibu magonjwa yote anataka maelezo zaidi kuhusu ugonjwa wako yeye atakupendekeza kwa zahanati ya kukusanya damu kwa ajili ya kufanya upimaji, kwa mfano, ili kukusanya na kupima damu. Daktari anayetibu magonjwa yote atakupatia pendekezo ili kuenda kwenye zahanati ya kukusanya damu.

↓

Peleka pendekezo lako kwenye zahanati ya kukusanya damu na upate vipimo.

Zahanati ya kukusanya damu itayatuma matokeo ya kipimo chako kwake daktari anayetibu magonjwa yote.

↓

Kulingana na matokeo ya kipimo chako unaweza kutembelea daktari anayetibu magonjwa yote tena.

↓

Ikiwa daktari anayetibu magonjwa yote hawezi kusuluhisha shida yako atakupendekeza kwa Daktari Mtaalamu. Watakupatia barua ya mapendekezo.

↓

Pigia simu kwa mtaalamu ili kupanga miadi na ubebe barua yako ya mapendekezo nawe.

## Shughuli

Andika maneno haya ya Afya katika lugha yako. Kijifurushi cha maelezo ya Afya yatakupatia vidokezo vingine.

| | |
|---|---|
| Daktari anayetibu magonjwa yote/daktari | |
| Mfumo wa utunzaji wa afya | |
| Mtaalamu | |
| Duka la dawa | |
| Maagizo | |
| Hospitali | |
| Dharura | |
| Daktari wa meno | |
| Miadi | |
| Dawa | |

# **Kitengo 5** Pesa

Hatua yako ya kwanza nchini Australia itakuwemo pamoja na kufungua akaunti ya benki na kupangia usaidizi wa muda mfupi wa kipesa kutoka kwa Centrelink. Sasa upo njiani kupata dola na senti za sarafu ya Australia pamoja na kufanya uamuzi kuhusu jinsi ya kusimamia malipo yako.

## Shughuli

Jifunze maneno machache ya Kiingereza kuhusu uwekaji wa pesa kwenye benki na sarafu ya Australia. Tafuta neno la Kiingereza kwa maneno haya ya kawaida ya benki. Kijifurushi cha maelezo kuhusu Pesa yatakupa vidokezo vingine.

| | |
|---|---|
| Akaunti hii hulinda pesa zako kutokana na wizi au kupotea. | |
| Nywila kwa ajili ya Mashine ya (Automatic Teller Machine - ATM) pamoja na manunuzi ya EFTPOS. Ni muhimu kuweka salama password hii mbali kutoka kwa watu usiojua. | |
| Kadi inayokuwezesha wewe kulipia bidhaa pamoja na huduma kwa kutumia pesa za mkopo. | |
| Mashine ambayo hukuwezesha wewe kutoa pesa kutoka akaunti yako ya benki kwa kutumia Nambari Ya Kibinafsi cha Kitambulisho (Personal Identification Number - PIN). | |
| Inawawezesha wanunuzi kulipia bidhaa kwa kutumia pesa walizonazo kwenye akaunti ya benki yao kwa kutumia kadi yao ya ATM badala ya kulipa pesa, katika biashara nyingi za rejareja. | |

### Sarafu ya Australia

Picha ya nani ipo juu kwenye uso wa noti ya $5.00 katika sarafu ya Australia? ______________________




Taja mnyama aliye kwenye uso wa peni ya $1.00 kwenye sarafu ya Australia ______________________



Mfanyikazi wa kesi au Mfadhili wako atakusaidia wewe kupata kutulia nchini Australia, lakini wewe unalo jukumu la jinsi unavyosimamia matumizi ya kipato yako ili kutekeleza mahitaji yako na maoni yako ya baadaye. Gharama ya maisha nchini Australia inaweza kuwa juu na kuishi kulingana na mpangilio wako wa matumizi ya pesa zako itakusaidia wewe kutimiza mahitaji na mipango yako ya baadaye.

Unafikiria ungependelea kununua nini unapowasili nchini Australia?

______________________________

______________________________

______________________________

## Shughuli

### Mpangilio wa matumizi ya pesa zako

Hii ni njia mojawapo ya kufikiria kuhusu mpangilio wa matumizi ya pesa zako. Orodhesha vitu kadhaa na uzitie kwenye sehemu tofauti. Baada ya miezi miwili inawezekana kuwa tofauti kwa hivyo jaribu mara nyingi tena unapotulia katika nyumba yako mpya.

| SASA | KATIKA MIEZI MIWILI |
|---|---|
| **Gharama zisizoweza kubadilika** – Gharama hizi lazima uzilipie wewe au shida zinaweza kutokea kwa wewe au jamii yako.<br>• ______<br>• ______<br>• ______<br>• ______ | |
| **Gharama zinaweza kubadilika** – Gharama hizi wewe unaweza kuzizuia ukitaka. Unahitaji bidhaa au huduma lakini unao uwezo wa kuamua utalipia pesa ngapi kwa kununua au kiasi gani utumie huduma hiyo.<br>• ______<br>• ______<br>• ______<br>• ______ | |
| **Ziada** – Gharama hizi wewe unaweza kuzizuia kamwe kama ukitaka. Si lazima kuzinunua lakini labda pia ungelipendelea kuwa nazo.<br>• ______<br>• ______<br>• ______<br>• ______ | |

# **Kitengo 6** Elimu

Unapofanya mipango yako ya kuhamia makao yako mpya nchini Australia, unaweza kutafakari kuhusu aina ya maisha ambayo unatarajia kuishi, aina ya kazi ambayo unaweza kupata au jinsi jamii yako itatulia katika jamaa mpya. Jukumu lako mwenyewe ni kujifunza Kiingereza na kuchukua nafasi za kuelimika ili itakusaidia wewe kutulia nchini Australia.

## Shughuli

Kijifurushi cha maelezo ya Elimu ya Shule itakupa wewe vidokezo vingine.

### Mpangilio wa elimu ya shule nchini Australia

| Kiwango | Umri (karibia.) | Daraja |
|---|---|---|
| Shule ya chekechea | 3-5 | haihusiki |
| Shule ya awali | 5-6 | haihusiki |
| Shule ya Msingi | 6-12 | 1-6 |
| School ya Upili /shule ya sekondari | 12-18 | 7-12 |
| **Kumbuka:** Katika majimbo mengine shule za msingi hufikia kikomo katika Mwaka wa 7 na Shule ya Upili huanza kutoka Mwaka wa 8. Uliza Mfanyikazi wa kesi au mshauri wako kuhusu maelezo zaidi. | | |

Kwa njia gani mfumo wa elimu nchini Australia ni sawa au tofauti na sehemu unapoishi sasa, au ulipoishi hapo awali?

Serekali inatoa elimu ya bure kwa watoto

Shule ya chekechea ni kwa watoto wa umri wa miaka minne

Elimu ya lazima kwa watoto wenye umri kati ya miaka tano na 17

Wasichana na wavulana wanahudhuria shule pamoja

Tunatarajia wazazi wahusike katika vipindi vya shule na elimu ya watoto wao

Nchini Australia, nafasi za elimu na ajira huwa zimekaribiana sana. Unapojitayarisha kuishi nchini Australia, ni mipango gani unayo wewe kwa mahitaji ya elimu yako?

## Shughuli

**Kupangia mafunzo na ajira yako ya baadaye**

Kijifurushi cha maelezo ya Elimu ya Watu Wazima kitakusaidia wewe katika shughuli hii.

Huduma hizi ni muhimu vipi kwako wewe?

| Huduma | Muhimu sana | Muhimu kidogo | Si muhimu sana |
|---|---|---|---|
| Kuhudhuria kosi ya AMEP | | | |
| Kukamilisha cheti cha shule ya sekondari katika chuo cha Ufundi na Elimu ya Ziada (Technical and Further Education - TAFE) | | | |
| Kumaliza kosi ya biashara au ustadi katika TAFE | | | |
| Kujiandikisha katika kosi ya chuo kikuu | | | |
| Kujiandikisha katika kosi baada ya Kuhitimu katika chuo kikuu | | | |
| Kuhudhuhuria kozi ya elimu ya Jamii | | | |

Ingawaje mfanyikazi wa kesi au mshauri wako atakusaidia wewe kupata huduma za elimu ya watu wazima, unayo mipango gani ili kukusaidia kuendelea? Utahitaji kuleta nawe nakala gani?

- 
- 
- 
- 
- 

Ni maswali gani uliyo nayo kuhusu elimu ambayo ungetaka kufuatilia wakati unapowasili nchini Australia?

- 
- 
- 
- 
- 

# **Kitengo 7** Ajira

Soko la kazi nchini Australia lina ushindani, na kazi hutuzwa kulingana na ustadi, sifa za uzoefu unaofaa na sifa itokanayo ya sifa ya kuhitimu. Ustadi wa lugha ya Kiingereza huthaminiwa sana. Wanabiashara na wataalamu wengi wanaweza kuhitajika kutumika katika kazi zisizohitaji ustadi wowote hadi wanapojifunza Kiingereza na kupata sifa zinazostahili zao kutambuliwa na kuongezeka kiasi fulani. **Kumbuka:** hii huchukua wakati fulani na kunazo huduma za serikali ambazo husaidia watu kujifunza Kiingereza na kupata kazi au mafunzo.

## Shughuli

Kijifurushi chenye maelezo kuhusu Ujira itakusaidia wewe kufanya shughuli hii.

Soma maelezo na utie alama ikiwa ni kweli au sio kweli.

| | | |
|---|---|---|
| 1. Jobactive yaweza kunisaidia kupata kazi | Kweli | Sio kweli |
| 2. Nitapokea usaidizi wa mapato wakati ninapowasili nchini Australia | Kweli | Sio kweli |
| 3. Mfanyikazi wa kesi yangu lazima anipatie kazi | Kweli | Sio kweli |
| 4. Ustadi wa Kiingereza ni muhimu kwa kupata kazi | Kweli | Sio kweli |
| 5. Watu wanaojitoa kwa hiari kwa kazi hulipwa | Kweli | Sio kweli |
| 6. Wewe hauhitajiki kulipa ushuru nchini Australia | Kweli | Sio kweli |
| 7. Wanaume na wanawake hutendewa sawa kazini | Kweli | Sio kweli |
| 8. Mara tu unapopata kazi wewe lazima ufahamishe Centrelink | Kweli | Sio kweli |
| 9. Kufika kazini kwa wakati sawa ni muhimu | Kweli | Sio kweli |
| 10. Watoto barubaru wanaweza kufanya kazi badala ya kuhudhuria shule | Kweli | Sio kweli |

## Shughuli

**Jifunze maneno kadhaa ya Kiingereza**

Haya ni baadhi ya maneno unayofaa kujifunza ili kuelewa mahitaji au matarajio mengine kuhusu ajira nchini Australia. Tafsiri maneno haya muhimu kwenye maneno ya lugha yako ili uwe na orodha inayofaa ya kumbukumbu wakati unapowasili nchini Australia.

Tax File Number __________

Bank account __________

Work experience __________

Interview __________

Reference __________

Qualifications __________

Volunteer __________

## Shughuli

### Kupangia kwa kupata kazi nchini Australia

Ungelipendelea kupata kazi ya aina gani nchini Australia?

Fanya kupanga mpango wa jinsi wewe unaweza kupata kazi hiyo.

| Ninazo hizi? | Ndio | La |
|---|---|---|
| Ustadi wa lugha ya Kiingereza | | |
| Sifa itokanayo na mafunzo kwa kazi ya aina hii | | |
| Uzoefu katika eneo la aina ya kazi hii | | |
| Kumbukumbu | | |
| Muhtasiri | | |
| Ustadi wa mahojiano | | |
| Ari ya kuitikia changamoto na vipingamizi | | |
| Maelezo jinsi ya utakavyopata kazi hii | | |

Andika maneno yoyote kuhusu mambo unayopendelea kufuatilia nchini Australia.

# **Kitengo 8** Sheria

Mila na desturi za watu huwasaidia kwa kuwapa njia ya kuona na kujichanganya duniani. Unapotulia nchini Australia, utapatana na njia tofauti za maisha na desturi. Hii inaweza kuwa mapambano, haswa kama mila na desturi zinapingana na mila na destiuri zako. Ni muhimu kukumbuka kuwa nchini Australia ina mfumo wa sheria za kidunia ambazo hutoa jamaa yenye usalama na usawa; jamii ambayo inatarajia watu kuwajibika kwa matendo na tabia zao.

## Shughuli

Sheria nchini Australia inaweza kuwa tofauti na zile za nchi zingine ambazo umeishi hapo awali. Tia alama kwenye chati hapo chini ili kuonyesha kuwa sheria nchini Australia ni sawa au tofauti. Tia alama kwenye mila na desturi zilizo na mapingamizi kwako. Kijifurushi cha maelezo ya Sheria za Australia itakusaidia kwa shughuli hii.

| **Sheria** | **Sawa** | **Tofauti** | **Pingamizi kwa mila na desturi zangu** |
|---|---|---|---|
| Sheria kuhusu kuwapa pesa maafisa wa serikali | | | |
| Sheria kuhusu jukumu la polisi | | | |
| Sheria za kidunia, zisizo sheria za kidini | | | |
| Sheria kuhusu vurugu za kinyumbani na kijamii na vurugu kama njia mojawapo ya adhabu | | | |
| Sheria kuhusu ubebaji visu na silaha zinginezo katika nafasi ya umma | | | |
| Sheria za kufunga ndoa | | | |
| Sheria kuhusu umri wa itikio la kisheria | | | |
| Sheria kuhusu unywaji wa pombe na uvutaji wa sigara | | | |
| Sheria kuhusu madawa ya kulevya | | | |
| Sheria kuhusu haki za usawa kwa wanawake | | | |
| Sheria kuhusu uendeshaji wa gari | | | |

**Andika maandishi yoyote kuhusu nini ungelipendelea kujua zaidi unapowasili nchini Australia. Kwa mfano:**

- Kituo cha polisi cha karibu sana na nambari za simu za kupigia simu katika wakati wa dharura
- Maelezo zaidi kuhusu sheria na uendeshaji wa gari
- Maelezo zaidi kuhusu jinsi ya kuwapa nidhamu watoto kulingana na sheria za Australia.

## Hadithi za kutulia

Australia imekuwa ikiwatuliza wakimbizi tangu Vita Vya Dunia 2, katikati ya karne iliyopita. Wamefanya mchango muhimu kwa maisha ya kijamii, kimatumaduni na kifedha ya watu wote wa Australia. Kila mmojawapo wa watu waliofanya makazi wanazo hadithi za kueleza kuhusu safari yao.

## Shughuli

Soma hadithi zilizotolewa kwako na mwalimu wa AUSCO na ujadiliane kuhusu safari yao na wenzako kwenye darasa lako.

Ni mapingamizi gani wamepitia?

Walifanya nini ili kujisaidia kupitia mapingamizi hayo?

Je, nini kinachofanana kwako na mtu katika hadithi ya makazi?

Je, hadithi yako ya makazi inasikika vipi?

## Rekodi ya ustadi

Unajihisia kujiamini kwa kiasi gani kuhusu kila ya mambo yanayofuata?

- Ikiwa unajihisi na matumaini sana tia kwenye sanduku alama ya ☒
- Ikiwa unajihisi unaelewa kiasi lakini unahitaji maelezo zaidi tia kwenye sanduku alama ⧄
- Ikiwa unafahamu kidogo sana au hufahamu lolote acha sanduku hilo bila kutia alama yoyote.

Hutarajiwi kuweka alama kwenye masanduku yote. AUSCO ni programu ya mwanzo kwa hivyo matokeo mengi ya kujifunza yatapatikana baada yako kupata uzoefu wa kuishi nchini Australia na kuhudhuria mifumo mengineo ya uanzilishi.

## Maelezo ya jumla ya Australia

| Je: | Je, unaweza: | Je, unaweza kufanya hivi: |
|---|---|---|
| ☐ unafahamu kuwa Kiingereza ni lugha ya taifa nchini Australia<br>☐ unafahamu kuwa Australia ni bara kubwa sana lenye hali tofauti ya maeneo ya anga<br>☐ unaelewa kuwa Australia ni jamaa yenye mchanganyiko wa mila iliyo na idadi kubwa ya watu wahamiaji<br>☐ unafahamu kuwa thamana ya demokrasia katika bunge la Australia<br>☐ unaelewa kuwa watu wa asili ya Aboriginal pamoja na watu wa visiwa cha Torres Strait wamekuwa wakiishi nchini Australia kwa karibia miaka elfu 50,0000 | ☐ kuuliza maswali kuhusu maarifa kuhusu maisha nchini Australia<br>☐ kutambua kuwa majimbo na wilaya ya Australia ikiwemo ni pamoja na jiji kuu<br>☐ kutambua kuwa historia za makazi katika nchini Australia<br>☐ kutaja baadhi ya tabia tofauti ambazo unaweza kuona nchini Australia<br>☐ kuelezea haki zako za kidemokrasia na jukumu, na jinsi uchaguzi unavyofanywa<br>☐ kutaja majina ya vyama muhimu vya kisiasa nchini Australia<br>☐ taja sikukuu muhimu nchini Australia na ueleze kwa nini zinasherekewa | ☐ kukamilisha mtihani wa uraia<br>☐ kujiandikiisha kupiga kura<br>☐ kupata maelezo kuhusu vyama vya siasa na jukwaa zao |

## Huduma za kutulia

| Je: | Je, unaweza: | Je, unaweza kufanya hivi: |
|---|---|---|
| ☐ unaelewa kuwa mpangilio wa makazi ni kwa muda mrefu<br>☐ unafahamu kuwa kunayo mapingano wakati wa kianzilishi cha kupata makazi<br>☐ unafahamu umuhimu wa kuomba usaidizi wakati unapohitajika<br>☐ unafahamu kuwa kunazo mashirika ya huduma ya serikali na ya jamaa yanayopatikana ili kusaidia watu kupata makazi<br>☐ unaelewa kuwa utapatiwa mfanyikazi wa kesi<br>☐ unaelewa kuwa kunazo kazi muhimu kadhaa ambazo wewe lazima utekeleze unapowasili nchini Australia | ☐ kutambua kazi muhimu ambazo wewe lazima utekeleze ndani ya wiki chache za kwanza unapowasili nchini Australia<br>☐ kueleza jukumu la wasaidizi wa kesi au washauri<br>☐ kutambua kuwa mashirika ya huduma ya serikali na ya jamii hupatikana ili kukusaidia kwa kupata makazi<br>☐ kutambua kuwa huduma zingine za kawaida zinaweza kupatikana katika jamii yako ya mtaa wako, kwa mfano, kilabu cha michezo, vikundi vya kijamii | ☐ kupata huduma za utafsiri na ukalimani<br>☐ kujaza maelezo ya kawaida kwenye fomu za rasmi<br>☐ kutumia usafiri wa umma<br>☐ kufungua akaunti ya benki<br>☐ kujiandikisha na Centrelink<br>☐ kujiandikisha na Medicare<br>☐ kujiandikisha katika programu ya Kiingereza |

## Nyumba

| Je: | Je, unaweza: | Je, unaweza kufanya hivi: |
|---|---|---|
| ☐ unaelewa kuwa kunazo aina tofauti za makazi zinazopatikana nchini Australia<br>☐ unaelewa kuwa lazima ulipe kodi ya nyumba ili kuishi katika makazi na gharama ya kukodisha nyumba ni tofauti katika maeneo tofauti ya Australia<br>☐ unaelewa kiwango cha makazi ambayo utaweza kulipia wakati unapotulia nchini Australia<br>☐ unaelewa kuwa ni jukumu lako wewe kufanya usafi na kupanga vyema nyumba yako<br>☐ unaelewa kuwa makazi yako nchini Australia ni ya muda mfupi tu na yataweza kupangiliwa na mfanyikazi wa kesi yako<br>☐ unaelewa kuwa watu ambao bado hawajafunga ndoa labda watahitaji kuishi na watu wengine nchini Australia | ☐ kutumia maneno muhimu yanayohusu mpangilio wa kukodisha nyumba<br>☐ kutaja vifaa vya nyumba ambazo wewe lazima una jukumu la kulipia<br>☐ kutaja mahali ambapo mali ya kukodisha imetangazwa<br>☐ kutaja haki na jukumu zako ukiwa kama mpangaji<br>☐ kutaja haki na jukumu za mpangishaji | ☐ kufanya utafiti na utambue makazi yanayokufaa wewe<br>☐ kujaza maelezo muhimu katika fomu za kukodisha<br>☐ kujiandikishe kwa vifaa vya nyumbani |

## Afya

| Je: | Je, unaweza: | Je, unaweza kufanya hivi: |
|---|---|---|
| ☐ unaelewa kuwa kunazo vipimo vya afya ambazo wewe lazima upate kabla na baada ya kuwasili nchini Australia<br>☐ unaelewa kuwa inapendekezwa sana kuwa watoto wapate chanjo<br>☐ unafahamu kuwa shule zingine huhitaji kumbukumbu ya orodha ya chanjo ya mtoto wakati kuonyeshwa wanapoanza shule ya utunzaji ya siku au shule ya kawaida<br>☐ unaelewa kuwa kunayo utunzaji wa kawaida wa bure au ruzuku kupitia mfumo unaoitwa Medicare<br>☐ unaelewa kuwa sio huduma zote za afya huwa bure kwa mfano udaktari wa meno na udaktari wa macho<br>☐ unaelewa kuwa afya huwa ni pamoja na afya ya akili na kunazo huduma za bure za ushauri ili kukusaidia wewe<br>☐ unafahamu kuleta nakala za matibabu yako nawe nchini Australia | ☐ kueleza ni wapi unapoweza kwenda kwa mahitaji ya makadirio ya afya wakati wa kutulia nchini Australia<br>☐ kueleza nini Medicare hulipa na nini hailipi<br>☐ kueleza tofauti zilizopo kati ya huduma za afya za umma na za kibinafsi ikiwemo ni pamoja na wajibu wa bima ya kibinafsi ya afya<br>☐ kuonyesha mpangilio wa huduma tofauti za afya ikiwemo ni pamoja na wakati na jinsi ya kuzipata<br>☐ kueleza thamana ya kuzuia magonjwa kwa kutumia chanjo<br>☐ kutambua huduma za afya ya akili na za ushauri zinazopatikana katika eneo la makazi yako | ☐ kukamilisha mahitaji ya makadirio ya afya yako unapowasili nchini Australia<br>☐ kujiandikishe na Medicare<br>☐ kuchukua jukumu lako kwa afya na ustawi wako na jamii yako<br>☐ kupigia simu huduma za dharura ikiwa utahitajika kufanya hivyo<br>☐ kupata huduma za afya zinazofaa kwa mahitaji yako<br>☐ kuwasiliana mahitaji yako ya afya kwako mwenyewe au kupitia huduma ya ukalimani |

## Elimu

| Je: | Je, unaweza: | Je, unaweza kufanya hivi: |
| --- | --- | --- |
| ☐ unaelewa wajibu wa AMEP<br>☐ unafahamu umuhimu wa kujifunza Kiingereza ili kupata elimu ya juu na ajira<br>☐ unaelewa kuwa mfumo wa elimu huwa ni pamoja na sekta ya umma na sekta ya kibinafsi<br>☐ unaelewa utofauti uliopo kati ya shule ya umma na shule za kibinafsi<br>☐ unaelewa kuwa elimu ya serikali ni bure<br>☐ unaelewa kuhusu majukumu ya wazazi katika elimu ya watoto wao<br>☐ unaelewa kuwa kunazo njia za elimu ya juu na elimu zaidi<br>☐ unafahamu kuwa wewe unaweza kupata cheti cha ustadi wako kutafsiriwa kwenye lugha ya Kiingereza bure bila malipo yoyote | ☐ kutumia maneno muhimu yanayohusu elimu<br>☐ kulinganisha na utofautishe mfumo wa elimu nchini Australia na mazoea yako mwenyewe<br>☐ kufanya uamuzi kuhusu shule ya watoto<br>☐ kueleza njia ambazo unaweza kutumia ili kupata elimu ya juu na elimu zaidi<br>☐ kutambua huduma za usaidizi unaopatikana kwa watu wanaotaka kusoma | ☐ kuhudhuria mahojiano ya wazazi na walimu ukisaidiwa na TIS<br>☐ kufanya utafiti, chagua na ujiandikishe kwenye kosi ya juu inayokufaa<br>☐ kuandikisha watoto katika shule ya mtaa na ukamilishe nakala zozote zile zinazohitajika<br>☐ kuelewa kuwa wazazi lazima wawape ruhusa kwa njia ya barua kwa shule ikiwa watoto hawatahudhuria shule<br>☐ kuelewa kuwa wakati wa likizo ya shule, pamoja na uweze kupanga shughuli ya watoto wako wenye umri wa kwenda shule wakati wa likizo |

## Sheria

| Je: | Je unaweza: | Je, unaweza kufanya hivi: |
|---|---|---|
| ☐ unaelewa kuwa watu wote wako sawa kulingana na sheria za Australia<br>☐ unaelewa uhuru gani unaolindwa na sheria za Australia<br>☐ unaelewa kuwa polisi waheshimiwe na siyo kuogopewa<br>☐ unaelewa kuwa aina yote ya mateso ya kinyumbani kwa jamaa na mateso ya kingono ni kinyume ya sheria na sheria hizi zinatekelezwa bila msamaha<br>☐ unaelewa kwamba maafisa ya serikali ya Australia ikiwa ni pamoja na maafisa wa polisi hawawezi kukubali zawadi au hongo<br>☐ unatambua kuna sheria kuhusu kumiliki na kuendesha gari la kibinafsi, kujamiiana, pombe, tumbaku, pamoja na vurugu<br>☐ unaelewa kwamba sheria za kidini haiwezi kutekelezeka kama inahitilafiana/kinyume na sheria za Australia | ☐ kutarajia kuwa vitendo ambazo zinaweza kuwa kinyume cha sheria katika Australia<br>☐ kutambua mashirika unayoweza kuwasiliana kama unahitaji msaada wa kisheria<br>☐ kuelezea aina ya unyanyasaji wa majumbani na nini inaweza kufanyika ili kukabiliana na unyanyasaji wa majumbani | ☐ kuwasiliana na polisi ikiwa upo matatani<br>☐ kuwasiliana na majenti ikiwa unahitaji usaidizi wa kisheria<br>☐ kuwasiliana na majenti ikiwa unahitaji usaidizi wa kusimamia maswala ya kinyumbani au kijamii |

## Ajira

| Je: | Je, unaweza: | Je, unaweza kufanya hivi: |
|---|---|---|
| ☐ unaelewa kuwa soko la kazi linalo mashindano<br>☐ unaelewa kuwa sifa zinazostahili kutoka ng'ambo zaweza kuitikishwa nchini Australia<br>☐ unaelewa umuhimu wa kujifunza Kiingereza ili kupata ujira<br>☐ unafahamu kuwa kazi hutuzwa kulingana na sifa njema za watu walio na uzoefu na sifa zinazostahili kazi hizo<br>☐ unaelewa haki na wajibu wa wafanyakazi katika Australia<br>☐ unaelewa taratibu ya maombi ya kazi na mahojiano<br>☐ unafahamu kuwa wewe unaweza kupata cheti cha ustadi wako kutafsiriwa kwenye lugha ya Kiingereza bure bila malipo yoyote | ☐ kutumia maneno muhimu yanayohusu ujira<br>☐ kufahamu nafasi kadhaa za ujira nchini Australia<br>☐ kueleza kuhusu njia za kutafuta ujira<br>☐ kuendeleza mazungumzo na mawasiliano yasiyo ya maneno wakati wa mahojiano ya ujira | ☐ kukamilisha maelezo yako kwenye ombi la kazi<br>☐ kuandika muhtasari na barua ya kuomba kazi<br>☐ kufanya utafiti kuhusu ujira kwenye tovuti<br>☐ kutafuta utambuzi wa sifa zinazostahili za nchi za ng'ambo |

## Pesa

| Je: | Je, unaweza: | Je, unaweza kufanya hivi: |
|---|---|---|
| ☐ unaelewa kuwa kuweka pesa kwenye benki kwa kutumia tovuti ni mazoea ya kawaida nchini Australia<br>☐ unafahamu gharama ya juu ya maisha nchini in Australia<br>☐ unaelewa wajibu wa mkopo katika jamii nchini Australia na unafahamu kuwa hatari inayohusika katika kupata deni<br>☐ unaelewa aina mbalimbali ya malipo ya Centrelink pamoja na kiasi cha malipo<br>☐ unaelewa mazoea ya kuweka pesa na taasisi ya kawaida kwenye benki nchini Australia | ☐ kutambua sarafu ya pesa za Australia na kuelewa thamana yake ukilinganisha na sarafu yako ya sasa hivi<br>☐ kufahamu nafasi zinazokuwezesha kupunguza matumizi nyumbani<br>☐ kutumia maneno muhimu yanayohusu pesa benki | ☐ kutumia mashine ya ATM na vifaa vya EFTPOS Ili kutoa pesa na kununua vitu<br>☐ kufanya mpangilio ya matumizi ya pesa nyumbani |

## Usafiri

| Je: | Je, unaweza: | Je, unaweza kufanya hivi: |
|---|---|---|
| ☐ unaelewa safari ya ndege kuelekea nchini Australia ni ndefu sana, na unaweza kulazimika kushuka katika kituo kingine kabla ya kuwasili<br>☐ unaelewa kuwa vifaa na huduma utakazopewa kwenye ndege<br>☐ unaelewa kuwa utapata kungojewa unapowasili katika uwanja wa ndege nchini Australia<br>☐ unaelewa nini unachoweza/ usichoweza kupeleka nawe nchini Australia | ☐ elewa maelezo yaliyopo hati ya usafiri<br>☐ kueleza maelezo kuhusu safari yako ya ndege<br>☐ kueleza mtindo wa kuondoka kutoka uwanja wa ndege ikiwemo pamoja na kujiandikisha, ulinzi, na uhamiaji<br>☐ kueleza mtindo wa kuwasili uwanja wa ndege ikiwemo pamoja na uhamiaji, kwarantini na kuchukua mizigo | ☐ kukamilisha kadi ya msafiri kuingia nchini Australia<br>☐ kupakia mzigo ambao unaitikishwa na sheria za uwanja wa ndege/ kampuni ya ndege na idara ya forodha na karantini nchini Australia |

Maelezo ya ziada

**Kwa Maelezo zaidi tafadhali wasiliana na AUSCO@dss.gov.au**

*Toleo la Marekebisho (Aprili 2018)*